



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI WA TARIME
(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi)



Simu Na.: +255 28 2690218
Nukushi: +255 28 2690218
Barua pepe: td@tarimetc.go.tz
Tovuti: www.tarimetc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji
S.L.P 45,
TARIME

Unapojibu tafadhali taja:
Kumb. Na. HMT/L:1/4/72

24 Mei, 2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Tarime kwa kuzingatia kibali cha Ajira chenye **Kumb. Na. FA. 97/288/01/9** cha tarehe **13/05/2022** kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR-UTUMISHI) anakaribisha maombi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za kazi;-

MTENDAJI WA MTA A III

Nafasi kumi na tano (15)

SIFA ZA MWOMBAJI

Awe amehitimu kidato cha nne (IV) au kidato cha sita (VI) mwenye mafunzo ya Astashahada/Cheti katika mojawapo ya fani zifuatazo:- **Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Jamii** kutoka katika Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

MAJUKUMU

- i. Afisa masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Mtaa.
- ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamiaji wa Utawala Bora katika Mtaa.
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Mtaa.
- iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Mtaa.
- v. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- vi. Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali.
- vii. Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaalam katika Mtaa.
- viii. Kusimamia ukusanyaji na kuhifadhi kumbukumbu zote za Nyaraka za Mtaa.
- ix. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi katika Mtaa.
- x. Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Mtaa.

MSHAHARA

Kwa kuzingatia ngazi ya mshahara ya Serikali TGS "B"

MASHARTI YA JUMLA

- i. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania wenye umri wa 18 hadi 45.
- ii. Mwombaji awasilishe picha moja ya hivi karibuni (Passprt size).
- iii. Mwombaji awasilishe maelezo binafsi (CV) inayojitosheleza yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu (3 referees)
- iv. Waombaji wote waambatishe nakala ya vyeti halisi vya masomo na taaluma (NTA-Level 5) na "Transcript" ya cheti cha taaluma, Cheti cha kuzaliwa na mwombaji atakayewasilisha "Results Slip", "Statement of Results", "Provisional Results" au "Transcript" bila nakala halisi ya cheti cha taaluma maombi yake hayatakubaliwa.
- v. Kwa waliosoma nje ya Nchi Elimu ya kidato cha nne na kidato cha sita wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Mtihani la Tanzania (NECTA).
- vi. Wote watakoachaguliwa kufanya usaili ndiyo watakoaitwa kwenye usaili (Interview).
- vii. Maombi yasiyozingatia vigezo vilivyoainishwa hayatahughulikiwa.
- viii. Maombi yaandikwe kwa mkono na yatumwe kwa njia ya Posta kupitia Anwani iliyotajwa hapo chini.
- ix. Mwombaji awe ni ambaye hajawahi kuajiriwa Serikalini.
- x. Mwisho wa kupokea maombi ni **tarehe 08/06/2022 saa 9:30 mchana.**

MUHIMU: Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya shule na vyeti vya taaluma.

MAOMBI YOTE YATUMWE KWA:-

MKURUGENZI WA MJI
HALMASHAURI YA MJI
S.L.P 45,
TARIME.

Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Halmashauri ya Tarime Mji [www.tarime tc.go.tz](http://www.tarime.tc.go.tz)



Gimbana E. Ntavyo
**MKURUGENZI WA MJI
TARIME**

